

102/3

KISWAHILI

FASIHI

Karatasi ya 3

Julai/Agosti - 2013

Muda: 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA SHULE ZA UPLI ZA WILYA YA TRANS-MARA MAGHARIBI

Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya.(K.C.S.E)

Kiswahili

Karatssi ya 3

Julai/Agosti

Muda 2 ½

MAAGIZO

- *Jibu maswali **manne** pekee*
- *Swali la kwanza ni ya **lazima***
- *Maswali hayo mengine **matatu** kutoka sehemu **nne** zilizobaki yaani, Riwaya , na **HADITHI**
*Fupi.tamthilia, fasihi Simulizi.**
- *Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.*

SEHEMU YA A: U SHAIRI.

1. LAZIMA

Soma shairi lifuatalo kwa makini,halafu ujibu maswali yanayofuatia.

Hakika **yamekithiri**, ni nani asoyajua?
Wazazi wayahubiri,na hivyo kutubagua
Hayana komwe fahari,ila kweli yatua.
Uhuru wa kuoana,ni lini tutaupata?

Mwanamke siyo huyo? baba mtu anasema
Mwanamke kwani huyo? anateta naye mama,
Sababu waitoayo, haina nguvu wima,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutampata?

Kabila letu nihili,sharuti uoe huko,
Unazomewa ukali,kuoa nje ni mwiko
Hivyo twafanywa **dhalili**,viumbe tuso mashiko
Uhuru wa kuoana ,ni lini tutaupata.

Wanachunguza tabaka,ndipo wazushe wahaka
Wauliza kwa haraka,wajue lake tabaka,
Wasioridhika wafika,arudi alikotoka,
Uhuru wa kuona, ni lini tutaupata?

Waichuja yake dini,ndo ndoa ibarikiwe
Lazima yake imani,iwe sawa na yakuwe
Huu kweli ni uhuru,wataka uondolewe,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Japo mwanipa elimu,uhuru ninautaka,
Na mie muniheshimu,nipate nilomtaka
Kuoita kitu adhimu, so mchezo kwa hakika
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Nawashauri wazazi,twahitaji kupumua,
Wawili ndo waamuzi , hata Mungu anajua,
Wasifu pasi ajizi, kwa yao njema hatua,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Ndoa ikivunjikana,wawili wajisakeni,
Isije kusemekana,wazazi ndio kiini,
Ndiposa hata Rabana,situtie lawamani,
Uhuru wa kuoana, ni lini tutaupata?

Aliye na masikio,mesikia kwa makini,

Tusitamani kilio, mithili tulo vitani,
Wakioa sema ndio. Mola asikulaani
Uhuru wa kuoana ni lini tataupata?

Maswali.

- a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (ala.1)
b) Shairi hili laweza kuwekwa katika bahari mbili. Zitaje huku ukitoa sababu (ala.4)
c) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipolitunga shairi hili?
d) Ni masharti gani kijana nafaa kuyatimiza kabla ya and oa na ambazo mshairi analalamikia Taja manne. (ala.4)
e) Vijana wanafaa kuchaguliwa mke/mume wa kuoa? Toa maoni yako. (ala.2)
f) Ukizingatia shairi ulilopewa eleza jinsi mtunzi alivyotumia uhuru wake. (ala.4)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (ala. 3)
(i) Wahaka
(ii) Yamekithiri
(iii) Dhalili.

SEHEMU YA B : RIWAYA

S.A Mohamed : UTENGANO

Jibu swali la 2 au la 3

2. Riwaya ya Utengano inadhihirisha vile kisasi kimekithiri katika jamii husika. Eleza kwa tafsihi ukitolea mifano mwafaka. (ala.20)
3. Si mchezo kwake kujaza chungu cha kumtoshia yeye na watoto wake na huyo Shoka, ambaye haleti chochote kwake lakini hodari wa kungoja kimeshapi kwa apandie”
- a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala.4)
b) Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili. (ala.4)
c) Eleza umuhimu wa kisa kinachorejelewa na dondoo. (ala.4)
d) Ukitumia mifano mingine katika riwaya ya Utengano, fafana maudhui mawili yanayodokezwa na dondoo hili. (ala.8)

SEHEMU YA C: TAMTHILIA

MSTAHIKI MEYA: Timothy M. Arege

Jibu swali la 4 au la 5

4. Mtu huvuna alichopanda. Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi”
- (a) Nani msemaji? Alimwambia nani? (alama 2)
(b) Nini kilichomfanya kusema hivyo? (alama 6)

- (c) Ukipanda pojo huwezi kuvuna kunazi” ina maana gani kulingana na muktadha matumizi yake? (alama 6)
- (d) Anayeambiwa alisema nini baada ya kuambiwa hivyo? (alama 2)
- (e) Taja matendo mengine manne ya kuonyesha kuwa walipanda pojo. (alama 4)

5. Jadili jinsi maudhui ya usaliti yanavyofafanuliwa katika tamthilia hii. (alama 20)

SEHEMU YA D : HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE:Ken walibora na Said A. Mohamed

6. Anwani ‘Shaka ya Mambo’ inaafikiana na matukio yote katika hadithi ya Shaka ya Mambo. Jadili. (ala. 20)

SEHEMU YA E : FASIHI SIMULIZI. (ALAMA 20)

- 7
- a) (i) Eleza maana ya kitendawili (ala.2)
- (ii) Eleza sifa bainifu za vitendawili. (ala 4)
- (iii) Eleza umuhimu wa vitendawili katika jamii (ala.4)
- b) (i) Nini maana ya mighani/migani . (ala.2)
- (ii) Fafanua sifa nne za mighani. (ala.8)

ANSWERS:

Order a copy of answers from www.schoolsnetkenya.com/order-e-copy

NB> We charge Kshs. 100 ONLY to meet website, e-resource compilation and provision costs